# MAOMBI

## Ya Kujikuza kiroho

TOLEO LA 5



BY DENIS & DEVIS JULIUS

# <u>MAOMBI MAALUMU YA KUJIKUZA KIROHO.</u>

**<u>~Toleo la tano</u>**

**UTANGULIZI.**

Haya ni maombi maalumu yanayolenga eneo la ukuaji kiroho. Sisi kama watoto wa Mungu, tunatarajiwa tukue toka daraja moja kwenda lingine kila siku. Ndivyo ilivyokuwa kwa Bwana Yesu, maandiko yanasema aliendelea katika "kimo na hekima". Kimo kinachozungumziwa hapo sio urefu wa mwili, bali ni kimo cha kiroho. Kutufundisha kuwa na sisi inatupaswa tuwe hivyo.

Ukuaji kiroho, hautokei ghafla tu ndani ya mtu. Mtu hawezi ishi maisha yaleyale tu ya wokovu, miaka miwili au mitatu, huonyeshi bidii yoyote,halafu akatarajia akue kiroho akidhani kuwa kuwepo kwake ndani ya Kristo tangu zamani ndio ukuaji wa kiroho, hapana. Anaweza akatokea mwingine aliyeingia ndani ya Kristo miezi miwili tu akawa mbali zaidi yake hata yeye uliyedumu kwa miaka kumi. Kwasababu yeye alizingatia kanuni za kiroho za ukuaji.

Kama tulivyotangulia kuona katika matoleo ya nyuma, kwamba Usomaji wa Neno, pamoja na Maombi ndio nguzo kuu mbili muhimu, na nyingine ni ibada. Lakini katika makala hizi tunaegemea zaidi katika eneo la maombi. Ikiwa utapenda kupata mafundisho ya Neno la Mungu basi tembelea website yetu hii www.wingulamashahidi.org utakutana nayo mengi zaidi ya 4,000. Au wasiliana nasi kwa namba zilizo mwisho wa makala hii.

Hivyo kila wiki tunakuwa na toleo jipya la mwongozo. Maombi haya ni ya SAA SITA (6), Kwa wiki. Ukizingatia kuviombea vipengele hivyo, Ni hakika kuwa zipo hatua usizozijua wewe za kiroho Mungu mwenyewe ataanza kukupigisha. Na ukiwa ni mtu wa maombi kama haya sikuzote yasiyokoma, wewe mwenyewe utaona tu baada ya kipindi Fulani mabadiliko makubwa katika maisha yako ya wokovu.

~Mwl Denis & Devis Julius

# <u>NGUZO KUU ZA KUINULIWA.</u>
**<u>~Toleo la tano</u>**

Katika biblia, tutaangazia mambo ambayo ni wazi mtu akiyazingatia hayo, basi atainuliwa juu sana kiroho , Kwasababu ndio mambo yaliyokuwa ndani ya Bwana na kwa mitume wake.

Mambo yenyewe ni haya.

1. **Neema,**
2. **unyenyekevu,**
3. **upole,**
4. **utii,**
5. **uaminifu.**
6. **Bidii**

## 1) <u>NEEMA.</u>(dk50)

Hii ni nguzo muhimu sana, kwa mtu yeyote kuitafuta usiku na mchana, na ndio ya kwanza.
Neema ni upendeleo mtu anaoupata asioustahili. Ni mfano wa mwanafunzi ambaye hajakidhi vigezo vya kuendelea kidato cha mbele, lakini anavukishwa hivyo hivyo tu. Ndivyo ilivyo katika maisha ya wokovu, tunategemea neema ya Kristo zaidi ya matendo yetu .
Mitume walitegemea sana, neema ya Mungu katika mambo yao yote, na ndio maana katika nyaraka zao zote, kwenye salamu waliwataka watu wote waongezewe jambo hili (Kwamfano ukisoma vifungu hivi utakutana nalo 1Wakorintho 1:3, 2Wakorintho 1:2, Waefeso 1:2 n.k.).

Nasi pia ili tukuzwe kiroho, yatupasa tuombe tuongezewe neema katika maeneo haya.

- ✓ **Neema katika karama zetu:** Zikue, zidhihirike, zilijenge kanisa
- ✓ **Neema katika kuhudumu:** Tushuhudiapo, tufundishapo, tuhubiripo watu wavutwe kwa haraka katika wokovu.
- ✓ **Neema ya kuomba:** Kiu ya kuomba maombi ya kujimimina sana mbele za Mungu.

*Zekaria 12:10 “Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya neema na kuomba; nao watamtazama yeye ambaye walimchoma; nao watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee; nao wataona uchungu kwa ajili yake, kama vile mtu aonavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza. 11 Siku hiyo kutakuwa na maombolezo*

*makuu huko Yerusalemu, kama maombolezo ya Hadadrimoni katika bonde la Megido"*

- **Neema katika kuachia nguvu za Mungu ndani yetu**: Uponyaji, ishara na miujiza. (Matendo 19:11-12, Matendo 4:29-31)

- **Neema katika kufunga**: Mifungo ya masafa marefu, inayovuviwa na Roho Mtakatifu (Mathayo 4:2)

- **Neema katika kusubiri:** Mwanadamu kwa asili si mvumilivu. Lakini Bwana ameahidi kuwaongezea nguvu wale wamngojeao. (Isaya 40:30-31)

## 2) <u>UNYENYEKEVU.</u> (dk50)

Unyenyekevu ni nguzo nyingine ya msingi inayompandisha mtu juu kwa haraka. Bwana Yesu alilijua hili ndio maana akaacha enzi na mamlaka akajishusha kuwa kama mtumwa.

*Wafilipi 2:7 bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; 8 tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba. 9 Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; 10 ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; 11 na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba*

Unyenyekevu, si kushushwa, bali kujishusha. Ni pale unapokuwa na uwezo wa kutumia mamlaka yako lakini hutumii. Kinyume cha unyenyekevu ni kiburi.
Daudi alijua umuhimu wa unyenyekevu na kwa huo akakuzwa,

*Zaburi 18:35b ".. Na unyenyekevu wako umenikuza"*

Haya ni maeneo ambayo unapaswa uombe unyenyekevu;

- **Unyenyekevu Kwa Mungu:** 1Petro 5:6 Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake
- **Unyenyekevu Kwa wanadamu:** Wapendwa wenzako, wafanyakazi wenzako, ndugu zako, na majirani zako, maboss wako. Uwaheshimu na kuwathamini.

## 3) **UPOLE.** (dk50)

Upole ni ile hali ya kuwa na uwezo wa kuchukua hatua ya adhabu kwa mamlaka uliyonayo, lakini hufanyi hivyo. Kwamfano sungura hali nyama hatuwezi kusema ni mpole, lakini simba mwenye uwezo wa kuwinda na kula nyama, anapoacha kufanya hivyo. Hapo ndio tunasema ni mpole.

Yesu aliye simba wa Yuda alikuja katika upole. Na vivyo hivyo sisi..

Hivyo haya ni maeneo ambayo tunapaswa tumwombe Mungu atukirimie.

- ✓ **Upole katika kunena.** (Wagalatia 6:1, Waefeso 4:2)
- ✓ **Upole katika mwenendo:**

*Yakobo 3:13 N'nani aliye na hekima na ufahamu kwenu? Na aonyeshe kazi zake kwa mwenendo wake mzuri, katika upole wa hekima*

- ✓ **Upole katika hisia:** Usiwe mwepesi wa kukasirika haraka, na kuchukua hatua.

## 4) **UTII.**(dk50)

Utii ni kukubali kufanya maelekezo au maagizo unayopewa kwa aliye na mamlaka ya juu zaidi yako, bila kujali yanakubaliana na maamuzi yako au la!

Mungu anamnyanyua mtu kwa haraka Yule mwenye kiwango cha juu cha utiifu. Haya ni maeneo ambayo tunapaswa tuombee Bwana atupe utiifu.

- ✓ **Utii kwa Mungu:** Kulitii Neno la Mungu, kuyashika maagizo yake yote (Yakobo 4:7, Waebrania 5:7-9)
- ✓ **Utii kwa wazazi:** Wakolosai 3.20 Ninyi watoto, watiini wazazi wenu katika mambo yote; maana jambo hili lapendeza katika Bwana.
- ✓ **Utii kwa mume:** Ikiwa wewe umeolewa, andiko linakutaka utiifu wako uwepo pia kwa mumeo 1Petro 3:1-6
- ✓ **Utii kwa kiongozi wako wa kiroho :** Filemoni 1:21
- ✓ **Utii kwa mabwana zetu (maboss):** Waefeso 6:5-8
- ✓ **Utii kwa wazee** : 1Petro 5:5
- ✓ **Utii kwa wenye mamlaka** : Tito 3:1-2

## 5) **UAMINIFU.** (dk50)

Tunapokosa uaminifu tunakosa kupandishwa daraja lingine bora. Bwana alisema maneno haya

*Luka 16:10 “Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia; na aliye dhalimu katika lililo dogo, huwa dhalimu katika lililo kubwa pia”.*

Musa alikuwa mwaminifu sana na ndio maana Mungu akamnyanyua katika viwango vile vya juu sana vya kiroho.

*Hesabu 12: 6 “Kisha akawaambia,Sikizeni basi maneno yangu;Akiwapo nabii kati yenu,Mimi,Bwana,nitajifunua kwake katika maono,Nitasema naye katika ndoto. 7 Sivyo ilivyo kwa mtumishi wangu, Musa; Yeye ni mwaminifu katika nyumba yangu yote; 8 Kwake nitanena mdomo kwa mdomo, Maana, waziwazi wala si kwa mafumbo; Na umbo la Bwana yeye ataliona. Mbona basi ninyi hamkuogopa Kumnenea mtumishi wangu, huyo Musa?”*

Hivyo hatuna budi kuyaombea maeneo haya:

- ✓ **Uaminifu katika kusimamia mambo madogo**
- ✓ **Uaminifu Katika kuifanya kazi ya Mungu**
- ✓ **Uaminifu katika Kuishi maisha matakatifu**
- ✓ **Uaminifu katika kuisimamia mali ya mwingine**

## 6) **BIDII**. (dk50)

Bidii ni kuongeza juhudi za dhati katika kufanya jambo Fulani. Ni ile hali ya kuongeza nguvu ya ziada juu ya jambo ambalo unaona lina umuhimu kwako kulifanya. Bidii yoyote huleta matokeo, hata ile ya ubaya, huleta matokeo mabaya, si zaidi ile nzuri?

Kinyume cha bidii ni uvivu. Vivyo hivyo na sisi rohoni, Bwana anataka tuwe na sifa hiyo. Hivyo licha ya kuidhihirisha, hatuna budi kuiomba Bwana atusaidie tuone umuhimu wa kumtafuta yeye.

*2Wakorintho 8:16 “**Lakini ahimidiwe Mungu atiaye bidii** ile ile kwa ajili yenu katika moyo wa Tito”*

Haya ni maeneo ambayo tunapaswa tumwombe Mungu atuongezee bidii ndani yetu;

- ✓ **Bidii katika kuwa amani na watu pamoja na utakatifu**

*Waebrania 12:14  Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao;*

- **Katika kuomba:**

*Yakobo 5:17  Eliya alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi, akaomba kwa bidii mvua isinyeshe, na mvua haikunyesha juu ya nchi muda wa miaka mitatu na miezi* sita.

- **Katika kusimimia kazi ya Mungu:** Warumi 12:8
- **Katika kusaidia wengine.** (kiroho&kimwili)
- **Katika kukesha.**
- **Katika kupendana.** (1Petro 4:8)
- **Katika kufanya kazi ya mikono.** (Waefeso 4:28)

Hivyo ukizingatia vipengele hivyo sita, kumwomba Mungu kwa urefu kabisa, kupata muda wa kutafakari na kumlilia yeye (Kila kipengele dakika 50, au zaidi), siku baada ya siku utakuwa unaona mabadiliko makubwa sana maishani mwako.

Bwana akubariki.

Kwa ushauri/ Msaada/ Maombezi wasiliana nasi kwa mawasilino haya;

Na, Mwl Denis & Devis Julius
Nuru_ya_ Upendo
Website: www.wingulamashahidi.org
Email: info@wingulamashahidi.org
+255693036618/ +255789001312